

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI

17 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 17 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KILIMO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA KILIMO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

244. MHESHIMIWA AHMED ALLY SALUM (SOLWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Katika Jimbo la Solwa tayari kuna maboma 158 ikiwemo Shule za Msingi, Sekondari na Afya na tayari tumeomba fedha ili kukamilisha maboma hayo:-

Je, ni kiasi gani cha fedha Jimbo hilo limepata ili kukamilisha maboma hayo.

245. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Handeni inahudumia karibu Majimbo manne lakini ina upungufu wa vifaa ambao unasababisha Wagonjwa wengi kupewa rufaa:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza vifaa ili Watu wengi wapate huduma.

WIZARA YA NISHATI:

246. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Zoezi la usambazaji wa umeme wa REA katika Wilaya ya Momba bado haujakamilika hadi sasa:-

- (a) Je, ni lini Serikali itanza mchakato wa kupeleka umeme katika Kata ambazo hazijafikiwa na miradi hiyo katika Jimbo la Momba;
- (b) Je, ni lini mradi wa kuwasha umeme Tarafa ya Kamsamba utakamilika.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

247. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kuna Wagonjwa wa kisukari, shinikizo la damu na kansa wanapata shida kubwa ya kiafya:-

Je, Serikali ina mpango gani katika kuwapatia huduma ipasavyo.

248. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Sera ya Wazee imeelekeza kuwapatia Wazee matibabu bure lakini utekelezaji wake haueleweki na pia una urasimu mkubwa:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa uhakika wa kuwaondolea kero na shida hizo wanazozipata Wazee katika suala zima la matibabu yao.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

249. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Daraja la Godegode limesombwa na maji wakati wa mvua za masika na daraja hilo ni kiungo kikubwa kati ya Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa ambalo ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapwa:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja hilo ili kurudisha mawasiliano kati ya Wananchi wa Kata za Godegode, Pwaga, Lumuma, Mbuga na Galigali.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

250. MHESHIMIWA DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF (MGOGONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja kazi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; moja ya kazi zake ni kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora:-

- (a) Je, kwa nini ripoti za Tume hiyo haziwekwi wazi kwa Umma;
- (b) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kujenga utamaduni wa ripoti hizo kujadiliwa Bungeni.



WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

251. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Magereza na Wananchi wa Kata ya Ukondamayo hususan Kijiji cha Tumaini umedumu kwa muda mrefu sasa:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kumaliza mgogoro huo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.



**DODOMA
17 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**